# Madiwani watakiwa kusimamia matumizi ya rasilimali za umma

**Na Shukuru Mgoba, Chunya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Chunya imewataka madiwani wa halmashauri hiyo kusimamia kwa uadilifu matumizi ya rasilimali za umma katika kata zao ili kuimarisha uwazi, utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa.

Wito huo ulitolewa na Kamanda wa Takukuru Wilaya ya Chunya, Francis Kisoma wakati akitoa salamu za taasisi hiyo kwenye mkutano wa baraza la madiwani wa kuhitimisha Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Kisoma alisema bado kuna changamoto katika baadhi ya kata na vijiji na wananchi wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kudhulumiwa haki zao, hivyo madiwani wana wajibu wa kusimamia masuala ya uadilifu na kuhakikisha wananchi wanatendewa haki.

Alisema madiwani wana nafasi muhimu katika uongozi wa halmashauri kwa kuwa ni wasimamizi wa uamuzi na matumizi ya rasilimali za umma na kamati mbalimbali za halmashauri zinaundwa chini ya usimamizi wao.

Alieleza kuwa nafasi hiyo inawapa madiwani jukumu kubwa la kuhakikisha rasilimali zinazopatikana katika halmashauri zinatumika kwa ufanisi na kwa manufaa ya wananchi, badala ya kutumiwa vibaya au kwa maslahi binafsi.

"Katika nafasi yenu mna jukumu kubwa katika suala la kuzuia na kupambana na rushwa, kama viongozi, mna wajibu wa kuhakikisha rasilimali za umma ndani ya halmashauri zinatumika vizuri kwa manufaa ya umma," alisema Kisoma.

Aliongeza kuwa madiwani wakisimamia ipasavyo matumizi ya fedha na rasilimali za umma, pamoja na kupinga ubadhirifu na kuhimiza uwazi na utawala bora, watakuwa sehemu muhimu ya kupunguza vitendo vya rushwa katika halmashauri.

Aliwataka pia kuwa mfano kwa wananchi kwa kuwahamasisha kutoa taarifa pale wanapobaini vitendo vya rushwa, ubadhirifu au ukiukwaji wa haki katika maeneo yao.

"Shida inapotokea na wananchi wakaona haki haitendeki, sheria hazifuatwi na uadilifu haupo, wengi hupoteza imani, ninyi kama viongozi katika maeneo yenu mnatakiwa kutengeneza mazingira ya kupokea malalamiko na kero za wananchi mnaowawakilisha," aliongeza.

Alitoa wito kwa madiwani kuunga mkono mpango wa Takukuru rafiki unaolenga kusikiliza kero za wananchi kwa kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa, akisisitiza kuwa jukumu hilo si la Takukuru pekee bali ni la jamii nzima.




Balozi wa Indonesia nchini, Tri Yogo Jatmiko (kushoto) akimkabidhi keki Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Kaffe Koffe, Muntazir Hussein wakati wa maadhimisho ya miaka 81 ya Uhuru wa nchi hiyo, hafla iliyofanyika Dar es Salaam jana. Kampuni ya Kaffe Koffe ndio wauzaji wakubwa wa kahawa kutoka Tanzania kwenda Indonesia (Picha na Mpigapicha Wetu).

# Ekari 603 za bangi zateketezwa Mvomero

**Na Zena Chande**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imebaini mbinu mpya zinazotumiwa na baadhi ya wakulima wa bangi, ikiwamo kuhama maeneo yaliyofikiwa na operesheni na kuingia ndani zaidi ya maeneo ya hifadhi ili kukwepa hatua za kisheria.

Hayo yamebainika katika operesheni maalumu iliyofanywa na DCEA Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro juzi.

Jumla ya ekari 603 za mashamba ya bangi zimeteketezwa, magunia 49 ya bangi yamekamatwa na watuhumiwa 13 wamekamatwa katika operesheni hiyo.

Akizungumza kuhusu operesheni hiyo, Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo alisema hatua hiyo ni sehemu ya mkakati endelevu wa serikali wa kudhibiti uzalishaji wa dawa za kulevya nchini.

Alisema operesheni hiyo iliyofanyika katika vijiji vya Misengele, Lugenge, Kisaki na Nyarutanga, pia ilibaini na kuharibu kambi 21 zilizokuwa zikitumiwa na wakulima wa bangi.

"Tumebaini kuwa baadhi ya wakulima wamehamishia shughuli zao ndani zaidi ya maeneo ya hifadhi ili kukwepa hatua za kisheria," alisema Lyimo.

Alisema hali hiyo si tu inaendeleza uzalishaji wa dawa za kulevya, bali pia inachangia uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji miti ovyo, uvamizi wa vyanzo vya maji na kuathiri mfumo wa ikolojia. Kwa mujibu wa Lyimo, tathmini ya operesheni zilizofanywa na DCEA tangu mwaka 2023 inaonesha kuwa licha ya mashamba mengi ya bangi kubainika na kuteketezwa Morogoro, baadhi ya wahusika wameendelea kubadilisha maeneo ya uzalishaji na kujificha ndani ya maeneo ya hifadhi.

Alisema hali hiyo inahitaji ushirikiano wa karibu kati ya DCEA, vyombo vya ulinzi na usalama, mamlaka zinazosimamia maeneo ya hifadhi na wananchi ili kuzuia maeneo hayo kutumiwa kwa uzalishaji wa dawa za kulevya.

Aliwataka wasimamizi wa maeneo ya hifadhi kuhakikisha maeneo yao hayatumiki kwa kilimo cha bangi na kusisitiza kuwa mamlaka itaendelea kufanya operesheni jumuishi nchini na kuendelea kutoa elimu kwa jamii na kuhamasisha wananchi kutoa taarifa kuhusu wanaojihusisha na uzalishaji, usafirishaji na biashara haramu ya dawa za kulevya.

# Wizara: AI isichukue nafasi uamuzi wa wataalamu elimu

**Na Veronica Mheta, Arusha**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Carolyne Nombo amesema matumizi ya akili unde (AI) katika mifumo ya elimu yanapaswa kuimarisha ubora na ufanisi wa tathmini badala ya kuchukua nafasi ya uamuzi wa kitaalamu wa wataalamu wa elimu.

Aidha, alisema mabaraza ya mitihani Afrika yawekeze katika usalama wa kidijiti, uchambuzi wa kina wa takwimu na zana zinazotumia AI kubaini udanganyifu na ukiukwaji wa taratibu za mitihani.

Profesa Nombo alisema hayo wakati akifungua Mkutano wa 42 wa Mwaka wa Shirikisho la Chama cha Tathmini ya Elimu Afrika (AEAA) uliohudhuriwa na wajumbe 2,352 kutoka nchi 28, ukiwa jukwaa la kubadilishana maarifa na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wataalamu, watafiti na watendaji wa tathmini ya elimu.

"AI inapaswa kuwa chombo cha kuongeza ubora na ufanisi wa tathmini ya elimu si kuchukua nafasi ya uamuzi wa kitaalamu wa wataalamu wa elimu," alisema.

Alisema AI inabadilisha kwa kasi ufundishaji, ujifunzaji, utafiti na tathmini, huku teknolojia hiyo ikitoa fursa ya kupata mrejesho kwa wakati na kuboresha mifumo ya upimaji huku akisisitiza Tanzania imejipanga vizuri kutumia AI pamoja na Tehama katika ujifunzaji huku akiendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi kupitia Samia Scholarship.

Hata hivyo, alisema matumizi ya teknolojia hiyo yameibua pia changamoto mpya, ikiwamo kulinda uadilifu wa mitihani ambapo kunahitajika mifumo madhubuti ya kuhakikisha teknolojia hiyo inatumika kwa kuzingatia maadili, uwazi, ulinzi wa taarifa, usawa na ujumuishi.

Profesa Nombo alitaka mabaraza ya mitihani Afrika kuwekeza katika usalama wa kidijiti, uchambuzi wa kina wa takwimu na zana zinazotumia AI kubaini udanganyifu na ukiukwaji wa taratibu za mitihani.

Aidha, alizitaka nchi za Afrika kuwekeza katika wataalamu na teknolojia zinazozalishwa ndani ya bara ili kubuni suluhisho za AI zinazozingatia mazingira na mahitaji ya Waafrika.

"Kama Waafrika, tunapaswa kulenga kuwaendeleza watu wetu watakaoweza kutengeneza suluhisho hizi na si kuwa watumiaji tu wa suluhisho hizo," alisema.

Alisema serikali inaendelea kuimarisha uwekezaji katika elimu, sayansi, teknolojia na ubunifu kwa lengo la kujenga nguvu kazi yenye ujuzi itakayowezesha nchi kuelekea uchumi wa kidijitali na unaotegemea maarifa.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Profesa Said Mohamed alisema mifumo ya elimu inapaswa kutafakari upya uhusiano wake na akili unde kutokana na kasi ambayo teknolojia hiyo inabadilisha ufundishaji, ujifunzaji na tathmini.

Alisema maendeleo ya haraka ya AI yameibua swali la msingi kuhusu iwapo mifumo ya sasa na ya baadaye ya elimu inahitaji teknolojia hiyo zaidi akieleza kuwa hiyo ni mabadiliko makubwa ya kimfumo na inaweza kuwa na nafasi katika kuamua ubora wa elimu.

Wakati huohuo, Rais wa AEAA, Dk Eshetu Gichoro alisema Afrika inahitaji kujenga mifumo huru ya tathmini ya elimu inayounganisha teknolojia na kuwa tayari kukabiliana na mahitaji ya baadaye.

Alisema teknolojia hiyo inaweza kusaidia katika upimaji unaozingatia uwezo wa mwanafunzi, uchambuzi wa utabiri na ujifunzaji unaolenga mahitaji ya mtu binafsi, ikiwamo kuongeza upatikanaji wa tathmini bora kwa jamii za vijijini na zilizotengwa.

Hata hivyo, Dk Gichoro alionya kuwa Afrika inaweza kuwa tegemezi kwa teknolojia zinazoagizwa kutoka nje ambazo huenda zisizingatie mazingira na mahitaji halisi ya mifumo ya elimu barani humo.